

'Tusilewe na Uhuru wa Watanganyika'

KWENYE mkutano wa hadhara uliofanyika katika uwanja wa Masiwani wa chama cha Frelimo Jumapili, Mwenyekiti wa wa Jimbo hili la Tanga wa chama hicho, Bi. Marcelina Sikava, aliuambia mkutano huo kwamba wanawake wa Ki-Msumbiji wamechoshwa na wanaume zao ambao wamekuwa wakidai Uhuru wa Msumbiji kwa muda mrefu bila kuwa na mafanikio yo yote.

Akasema kuwa sasa ni wajibu wa mwana Msumbiji ye yote nchini Tanganyika na

Ripota wetu Tanga

po pote pale nje ya Msumbiji kila akaapo, akifanya kazi, akila, akilala, afikirie dhiki zinazowapata ndugu wananchi walioko Msumbiji na wala asikae tu akilewa na raha za Uhuru wa wenzake.

Akasema. "Sisi wanawake tumechoshwa na uongozi wenu sasa tuachieni sisi tuji-vike silaha twende tukapigane na Mreno ili tutokoe nchi yetu".

Mwanamke huyo akaendei-ea kusema kuwa sasa sio

wakati tena wa wananchi wa Msumbiji kusema maneno tu kila siku bali ni wakati wa kuungana na kuwa kitu kimoja na kupigania leoleo hii na kwenda kumwondosha Mreno kwa "ngumi".

Akasema kuwa katika vita vya kudai uhuru wa Msumbiji kusiwe na mambo ya kuwekana nyuma nyuma bali mume akiwa mbele lazima na mkewe awe nyuma yake tayari kwa lo lote litakalotok- ea. Akaonya kuwa ingawa nchi ya Tanganyika ni kari- mu kwao lakini wananchi wenyewe wasilewe na ukari- mu huo na kusahau kuiokoa nchi yao kusudi hapo kesho nao waje wawafanye wana Tanganyika ukarimu.